

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA MOJA

16 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA MOJA – TAREHE 16 APRILI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

84. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itazikarabati barabara za Jimbo la Mwibara ambazo zimeharibika ili kuruhusu mawasiliano kwa Wananchi.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

85. MHESHIMIWA STANLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaweka taa katika barabara kuu ya Mji wa Maswa.

86. MHESHIMIWA KASSIM IDDI IDDI (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Geita – Bukoli hadi Kahama kwa kiwango cha lami.

87. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Makofia kupitia Mlandizi hadi Vikumbulu Kisarawe.

WIZARA YA KILIMO:

88. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-
Pamoja na Kyerwa kuwa na Wakulima wengi wa Kahawa bado soko linakuwa gumu:-

Je, ni lini Serikali itafikiria kubadilisha mfumo wa ununuzi wa Kahawa kwa Wakulima.



WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

89. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini utekelezaji wa mradi wa kuendeleza Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (*REGROW*) utaanza.

**90. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA
(MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza mgogoro kati ya Hifadhi ya Ruaha na Wakulima na Wafugaji wanaozunguka Hifadhi hiyo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**91. MHESHIMIWA AHMED YAHYA
ABDULWAKIL (KWAHANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itawaunga mkono Wananchi wa Chukwani waliojitolea kujenga Kituo cha Polisi cha gorofa moja kwa kumaliza ujenzi wa Kituo hicho.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**92. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ipo tayari kupitia upya Sera na Sheria ya Uvuvi nchini ambayo inaonekana kutokidhi mahitaji ya Wavuvi wadogo.

WIZARA YA MAJI:

**93. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya maji katika Mkoa wa Katavi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
16 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**